

Shughuli za Njoo, Unifuate

Kwa ajili ya jioni ya nyumbani au kujifunza maandiko—au kwa ajili ya burudani tu!



Februari 26–Machi 3

Mahekalu ya karatasi

KWA AJILI YA 2 NEFI 11–19

Isaya alifundisha kwamba mahekalu ni sehemu maalumu ambapo tunajifunza kuhusu Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo (ona 2 Nefi 12:3). Tengeneza hekalu lako mwenyewe! Kunja kipande cha karatasi katika theluthi. Kata mwisho mmoja katika pembe tatu. Kunjua karatasi ile na ujichore mwenyewe hapo katikati.

Kwa ajili ya watoto wadogo: Tazameni picha ya hekalu pamoja. Zungumza jinsi mnavyoweza kuhisi upendo katika nyumba ya Mungu kama vile tu katika nyumba yenu wenyewe.

Machi 4–10

Shuhuda za Kuimba

KWA AJILI YA 2 NEFI 20–25

Isaya alishiriki ushuhuda wake juu ya Yesu Kristo. Alisema Yesu alikuwa nguvu yake na wimbo wake (ona 2 Nefi 22:2). Ni nyimbo zipi kuhusu Yesu unazozipenda? Zungumza kuhusu kwa nini unazipenda. Kisha ziimbeni pamoja!

Kwa ajili ya watoto wadogo: imbeni pamoja “Tell Me the Stories of Jesus” (*Kitabu cha Nyimbo za Watoto*, 57). Mruhusu mtoto wako anyanyue juu picha ya Yesu kila wakati anapotajwa katika wimbo.



Machi 11–17

Mstari juu ya Mstari

KWA AJILI YA 2 NEFI 26–30

Baba wa Mbinguni hutusaidia sisi tujifunze “mstari juu ya mstari,” au kidogo kidogo kwa wakati (2 Nefi 28:30). Kwa pamoja, simulieni hadithi pendwa ya maandiko mstari mmoja kwa wakati! Kila mtu anachukua zamu kusema sentensi moja ya hadithi mpaka hadithi imalizike.

Kwa ajili ya watoto wadogo: Baba wa Mbinguni hutusaidia tujifunze kuhusu Yesu Kristo. Nenda kwenye ukurasa wa 48 na mfanye zamu kupaka rangi sehemu ya picha kwa wakati.



Machi 18–24

Hatua za Kumfuata Yesu

KWA AJILI YA 2 NEFI 31–33

Nefi alifundisha kwamba tunamfuata Yesu Kristo wakati tunapokuwa na imani katika Yeye, kutubu, kubatizwa, kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu na kuvumilia hadi mwisho (ona 2 Nefi 31). Andika kila hatua kwenye kipande tofauti cha karatasi, kisha vitandaze sakafuni. Mtu mmoja anafumba macho yake na kuhesabu mpaka 10 huko kila mtu mwingine anasimama juu ya karatasi. Mtu aliyehesabu kisha anasema mojawapo ya hatua za kumfuata Yesu. Mtu aliyesimama juu ya karatasi hiyo kisha atahesabu.

Kwa ajili ya watoto wadogo: Tunapokuwa na imani katika Yesu Kristo, tunafuata kile Yeye anachosema. Unda mstari na mtembee kwenye eneo mlipo. Mtu aliye mbele ndiye kiongozi. Kila mtu anaigiza jinsi kiongozi anavyotembea. Fanyeni zamu kuwa kiongozi!



Machi 25–31

Yungiyungi za Pasaka

KWA AJILI YA PASAKA

Kwa sababu ya Yesu Kristo, sisi pia tutaishi tena baada ya kufa (ona Alma 40:22–25). Tengeneza kazi ya mikono ya yungiyungi ya Pasaka iliyo kwenye ukurasa wa 17. Weka yungiyungi zako mahali ambapo familia yako inaweza kuziona ili kuwasaidia wamkumbuke Mwokozi wiki hii.

Kwa ajili ya watoto wadogo: Someni kuhusu Pasaka kwenye ukurasa wa 46. Waruhusu watoto wako waoneshe kwa kidole kila picha ya Yesu wakati mnaposoma.